

## **KISWAHILI KIDATO -CHA PILI**

**MEI 2020**

### **1. Ufahamu (al. 15)**

#### ***Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali***

Uongo ni kinyume cha ukweli. Katika dunia hii tuishio, ni watu wachache tu ambao si waongo. Watu wanapotaka kudanganya au kuwapunja wengine hutumia uongo. Licha ya kuwa uongo huweza kumsaidia mtu kujiokoa pengine, ni tabia mbaya na si kitu cha kupendelea wala kupendeza maishani. Uongo hautumiwi na watu waovu na wajinga peke yao, bali hata watu wema huutumia. Hata hivyo, ni muhimu kujua kuwa uongo ni bahari hatari sana katika dunia hii. Mwongo mmoja huweza kupoteza na kuangamiza watu kadha wa kadha. Uongo wa wajinga hugunduliwa sana kuliko ule wa wataalamu. Baadhi ya madhara hutokea duniani kutokana na uongo wa watu wakubwa kuliko ule wa watu wadogo. Lakini lazima tukumbuke kuwa uongo ni kama giza, hukimbia mbele ya cheche ndogo ya nuru ya kweli. “uongo hukimbia kweli ikidhiri” ni methali ya Kiswahili ikumbushayo watu udhaifu wa uongo. Uovu mkubwa wa uongo ni kujidanganya mwenyewe kuwa uongo wako hautagunduliwa, bila ya kujua njia ya mwongo ni fupi.

(Kimenukuliwa na kuhaririwa upya kutoka S.Robert, 'Uongo' Insha na Mashairi).

Maswali

- (a) Kipatia kifungu ulichosoma anwani mwafaka. (al. 1)
- (b) Ni watu gani ambao hutumia uwongo? (al. 2)
- (c) Ni kwa nini uongo ni hatari? (al. 1)
- (d) Kwa maoni yako kwa nini uongo wa wajinga hugunduliwa kuliko wa wataalamu? (al. 2)
- (e) Ni madhara gani makubwa yanayotokana na uongo? (al. 2)
- (f) Kulingana na mwandishi, je kifungu hiki kinatufunza nini? (al. 2)
- (g) Eleza maana ya msamiati ufuatao.
- (i) bahari – uwanja mk\_\_\_\_\_
- (ii) madhara -
- (iii) cheche –
- (iv) udhaifu –

### **2. Sarufi na matumizi ya lugha . (al. 30)**

- (i) Taja ata mbili kuu zinazotumika kuamkia irabu. (al. 2)
- (ii) Taja irabu mbili zinazotamkwa ulimi mbele midomo ikiwa imetandazwa. (al. 2)
- (b) Andika vipashio vine vya lugha ya Kiswahili. (4 mks)
- (c) Onyesha viambishi katika kifungu kitenzi kifuatacho. (al. 3)  
Waliolima \_\_\_\_\_
- (d) Weka shadda katika neno lifuatalo kulipa maana mbili tofauti barabara. (al. 2)
- (e) Onyesha nomino zilizopigiwa mstari ni za aina gani  
Wanafunzi walisafiri hadi Nairobi na wakakutana na wabunge waliokuwa wanaelekea pwani.  
(al.
- (f) Tunga sentensi mbili kuonyesha maana ya vitate vifuatavyo. (al. 2)  
Ndoa / doa

(i)

(ii)

(g) Akifisha sentensi ifuatayo: (al. 2)

ukimwona mama kilonzo siku ya jumapili mwambie tukutane webuye leo jioni

(h) Weka nomino zifuatazo katika ngeli zake (al. 2)

(i) mtume –

(ii) mvua –

(i) Bainisha maneno katika sentensi ifuatayo. (al. 3)

Mwalimu na mwanafunzi mmoja wataenda haspitalini

(j) Weka nomino ifuatayo katika ukubwa na kisha udogo wake. (al. 2)

Nyoka

(k) Andika sentensi zifuatazo katika hali timilifu wakati uliopita. (al. 2)

(i) Wasukuma alichanga viazi

(ii) Nyanya analima shamba lake. (al. 2)

(l) Sahihisha sentensi zifuatazo: (al. 2)

(l) Ushanga ambayo alinunuliwa hutamfaa.

(ii) Nywele ambayo imenyolewa itatupwa.

Fasihi Simulizi (al. 5)

1. Eleza vipera vifuatavyo vya hadithi.

(i) Mighani -

(ii) visasili –

2. Eleza umuhimu wa hadithi za fasihi simulizi katika jamii.

(i)

(ii)

(iii)